# GRADE 6 KPSEA NATIONAL PRE MOCK 3

**Kenya Primary School Education Assessment**

# KISWAHILI

## MUDA: SAA 1

**SOMA KIFUNGU KIFUATACHO KISHA UJIBU MASWALI I HADI 5.**

(Ni alasiri Nafula na Yohana wamekutana Kambini. Ni msimu wa masika)

Nafula : (kwa huzuni) Hujambo mwenzangu?

Yohana : Sijambo. U hali gani?

Nafula : Si njema kwa sababu ya hali tuliyomo sasa.

Yohana : Usijali mwenzangu, tumtumainie Maulana kwa yote.

Nafula : Ulifika lini hapa? Na hali ilikuwaje kule ulikotoka?

Yohana : Nilifika juzi kwa kuokolewa na wahisani wa msalaba mwekundu baada ya makaazi yetu kusombwa na maji.

Nafula : Mimi na nina yangu tuliwasili jana tukiwa tumeokolewa na walinda usalama.

Yohana : Kwa yote tumshukuru Mola kwa kutuokoa.

Nafula : Amina

1. Watu husabahiana hujambo wakati gani?
   A. Wakati wowote
   B. Machweo
   C. Asubuhi
   D. Adhuhuri
2. Nafula na yohana walipokutana walikuwa katika hali gani?
   A. Furaha
   B. Majuto
   C. Kuomboleza
   D. Kusherehekea
3. Kulingana na mazungumzo jina jingine la Mola ni?
   A. Subuhano
   B. Jalali
   C. Maulana
   D. Rabuka
4. Msimu wa jua kali bila mvua huitwa _____
   A. Vuli
   B. Kiangazi
   C. Masika
   D. Kipupwe
5. Kulingana na mazungumzo athari za mafuriko ni zipi?